# HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)


MKOA WA RUVUMA

Anwani ya Simu: "NYASA COUNCIL"
Ofisini Simu Na: 025 -2952003
Fax Na: 025 -2952005
Nyumbani: 025 -
*Barua pepe:- ps.ded@nyasadc.go.tz*
Unapojibu tafadhali taja:

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S. L. P. 90,
MBAMBA-BAY,
RUVUMA.


**Kumb.Na.NDC/C.10/6/3** **23/12/2017**

## Kwa Wananchi Wote,

Yah: **MWALIKO WA KUSHIRIKI TAMASHA LA UTALII WILAYANI NYASA LITAKALOFANYIKA KUANZIA TAREHE 01/01/2018 HADI TAREHE 06/01/2018**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu,

Wilaya ya Nyasa ilianzishwa tarehe 08/03/2012 kwa Tangazo la Gazeti la Serikali Na.87. Wilaya ya Nyasa ina eneo lenye ukubwa wa Kilomita za mraba 6,790 Kusini Magharibi mwa Mkoa wa Ruvuma. Wilaya ya Nyasa inapakana na Wilaya ya Mbinga na Songea upande wa Mashariki, Nchi ya Malawi upande wa Magharibi, na Nchi ya Msumbiji upande wa Kusini na Wilaya ya Ludewa (Mkoa wa Njombe) Kaskazini.

Wilaya ina sifa ya kuwa na mvua za kutosha na joto maeneo ya mwambao mwa Ziwa na Baridi kali maeneo ya milimani. Mvua huanza mwezi Desemba hadi Aprili/Mei zinazokadiriwa kunyesha kati ya mm 800 na mm 1,224.

Ili kukuza Sekta ya Utalii na kutangaza fursa za uwekezaji hapa nchini Tanzania na hususani Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma; Uongozi wa Wilaya na Halmashauri kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Nyasa, uliamua kuanzisha Tamasha la Utalii Wilayani Nyasa ili kuvitangaza Vivutio vya Utalii vilivyopo na kutumia tamasha hili kutangaza fursa nyingi za uwekezaji katika Sekta za Uvuvi, Kilimo na Viwanda; ambapo Tamasha la Kwanza lilifanyika tarehe 27/12/2016 hadi tarehe 30/12/2016, kwa ufanisi mkubwa.

Mwaka huu Tamasha linafanyika kuanzia tarehe 01/01/2018 hadi tarehe 06/01/2018 ambapo Mgeni Rasmi ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa.

Miongoni mwa vivutio vya Utalii vilivyomo Wilayani Nyasa ni pamoja na Ziwa Nyasa lenye Visiwa vya kuvutia, mawe yenye umbo na rangi mbalimbali za kuvutia, Fukwe safi zenye mchanga wa rangi mbalimbali (nyeupe, mchanga mfinyanzi, kahawia, fukwe za mawe). Aidha Ziwa limetokana na Bonde la Ufa na hivyo kulifanya kuwa na tabia nyingi zisizopatikana duniani kwingine (mfano; Mawimbi Nyumba au kutulia mithili ya sakafu). Ziwa lina aina mbalimbali za Samaki wa Mapambo zaidi ya aina 403 ambazo hazipatikani sehemu nyingine yoyote Duniani.

Vivutio vingine vilivyopo ni Bonde la Ufa, Safu za Milima ya Livingstone, Maporomoko ya Maji, mapango katika mawe makubwa yaliyomo Ziwani, Pori la Akiba la Liparamba lenye Wanyama kama vile Simba, Chui, Tembo, Tandala Wakubwa, Viboko, Mamba, Nyati, Mbuzi Pori nk.

Kwa upande wa fursa za uwekezaji Wilaya ina mazingira mazuri ya kuwekeza katika Hoteli za Kitalii, Fukwe, Maeneo ya Kujenga Viwanda Vikubwa na Vidogo katika Sekta za Kilimo na Uvuvi. Katika kilimo mazao mengi yanastawi vizuri sana kama vile mazao ya biashara (Kahawa, Korosho, Kakao; vilevile mazao ya chakula na biashara kama mahindi, mpunga, mihogo, ufuta, karanga, maharage na ndizi.

Wilaya imejaliwa kuwa na Misitu ya Asili inayofaa kwa ufugaji wa nyuki na baadhi ya misitu hii hutumika kama maeneo ya kuzaliwa kwa ndege wanaohamia toka barani Ulaya kwa msimu wa kuzaa.

Wilaya ya Nyasa pia inayo madini mengi ikiwemo ya dhahabu katika Eneo la Dar Pori mpakani na Nchi ya Msumbiji.

Wilaya ya Nyasa inavutia pia kwa kuwa inapakana na nchi mbili za Msumbiji na Malawi. Wilaya inazo Bandari za Mbamba bay, Liuli, na Ndumbi kwa ajili ya uchukuzi na usafirishaji wa mizigo katika Ziwa Nyasa na hivyo kurahisisha biashara ya kimataifa.

Wilaya ya Nyasa pia ni maarufu kwa Kilimo cha Matunda kama vile Maembe, Mananasi, Ndizi, Limao, Mapera na Mapapai.

Wilaya ya Nyasa ina Ziwa na Mito inayotoa Samaki wenye ladha nzuri zisizopatikana katika Maziwa na Mito mingine hapa Nchini na Duniani kote.

Utamaduni wa wana-Nyasa ni mpana sana na wenye kuvutia na hususani katika Ngoma za asili kama vile Mganda, Kioda, Lindeku n.k. Wenyeji ni wakarimu kwa asili na wamefanikiwa kutoa wasomi wengi hapa nchini katika sekta mbalimbali za sayansi, uchumi na jamii.

Ndugu Mtanzania; nakuomba shiriki nasi katika Tamasha la Utalii Nyasa ili kutusaidia sisi kufanikisha Tamasha hili na kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano katika kukuza Sekta ya Utalii na Uwekezaji kuelekea Uchumi wa Viwanda na Ushindani wa Masoko ya bidhaa zetu Kitaifa na Kimataifa.

Napenda kukukaribisha wewe mdau muhimu; njoo ***"kuwekeza, kuimba, kucheza, kuogelea, kula samaki wetu, dagaa na kunywa kahawa yetu inayouzika kwa faida".***

Kumbuka kuwa Mgeni Rasmi katika Tamasha hili ni Mh. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa.

Nakutakia Maandalizi mema na safari njema kuja kushiriki nasi katika Tamasha la Utalii Nyasa.

Karibuni sana.

MKURUGENZI MTENDAJI (W) S.L.P 90, MBAMBA BAY HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA

Dkt. Oscar Albano Mbyuzi
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

Nakala: Katibu Tawala (M),
S.L.P. 74,
**SONGEA - RUVUMA**

" Mhe. Mbunge Eng. Stella Martin Manyanya,
S.L.P. 90,
**NYASA.**

Mkuu wa Wilaya,
S.L.P 01,
**NYASA.**